ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 16*** ***18th April, 2025***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 16 Vol. 106 Dated 18th April, 2025*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

## KANUNI ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI ZA MWAKA 2025

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 162 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024)*

***Anwani ya Simu**: "UCHAGUZI"*
***Nambari ya Simu:** +255 26-2962345-8*
***Nambari ya Nukushi:** +255 26-2962348*
***Baruapepe:** uchaguzi@inec.go.tz*
***Tovuti:** www.inec.go.tz*

*Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,*
*Uchaguzi House,*
*Eneo la Uwekezaji Njedengwa,*
*Kitalu D, Kiwanja Na. 4,*
*5 Barabara ya Uchaguzi,*
*S.L.P 358,*
***41107 DODOMA.***

**Aprili, 2025**

# YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................ iv
SEHEMU YA KWANZA ........................................ 1
1.0 Jina, Lengo, Matumizi, Wahusika na Wajibu wa Kusaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za Mwaka 2025 ........................................ 1
1.1 Jina la Kanuni ........................................ 1
1.2 Lengo la Maadili ........................................ 1
1.3 Muda wa Kutumika kwa Kanuni za Maadili ........................................ 1
1.4 Wahusika wa Kanuni za Maadili ........................................ 1
1.5 Wajibu wa Kusaini na Kuthibitisha Kuheshimu Kanuni za Maadili ........................................ 2
SEHEMU YA PILI ........................................ 3
2.0 Maadili kwa Vyama vya Siasa na Wagombea katika Kuendesha Shughuli za Siasa Wakati wa Kampeni hadi Kutangazwa kwa Matokeo ........................................ 3
2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea ........................................ 3
2.2 Mambo Yasiyotakiwa Kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea ........................................ 7
2.3 Maadili Wakati wa Upigaji Kura Hadi Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi ........................................ 10
SEHEMU YA TATU ........................................ 14
3.0 Maadili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ........................................ 14
3.1 Wajibu wa Serikali ........................................ 14
3.2 Yasiyotakiwa Kufanywa na Serikali ........................................ 15

3.3 Mambo Yasiyotakiwa Kufanywa na Watendaji wa Serikali Wakati wa Uchaguzi ........ 15
SEHEMU YA NNE ........ 17
4.0 Maadili kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ........ 17
4.1 Yanayotakiwa Kufanywa na Tume ........ 17
4.2 Yasiyotakiwa Kufanywa na Tume ........ 19
SEHEMU YA TANO ........ 20
5.0 Usimamizi na Utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi ........ 20
5.1 Kamati za Maadili ........ 20
5.2 Muundo na Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ........ 20
5.4 Kamati za Maadili Wakati wa Uchaguzi Mdogo ........ 23
5.5 Uwasilishaji wa Malalamiko ........ 24
5.6 Muda wa Kuwasilisha Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili ........ 24
5.7 Kuitisha Kikao cha Maadili ya Uchaguzi ........ 24
5.8 Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko ........ 24
5.9 Rufaa Dhidi ya Uamuzi wa Kamati ........ 26
5.10 Malalamiko Dhidi ya Tume, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ........ 27
5.11 Malalamiko Dhidi ya Serikali ........ 28
5.12 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi Ngazi ya Kitaifa, Jimbo na Kata Katika Kutoa Adhabu ........ 28
5.13 Mamlaka ya Kamati ya Rufaa ya Maadili ya Uchaguzi ........ 30
5.14 Kushindwa Kutekeleza Maadili ........ 31
5.15 Uamuzi wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili Kutoathiri Haki ya Kufungua Shauri la Uchaguzi ........ 31
SEHEMU YA SITA ........ 32

6.0 Tamko la Kukubali Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ..................... 32
6.1 Tamko la Serikali ..................................................................... 32
6.2 Tamko la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ................................ 33
6.3 Tamko la Viongozi wa Vyama vya Siasa ...................................... 34
SEHEMU YA SABA ......................................................................... 35
7.0 Kufuta Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 ............................... 35

# KANUNI ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2025

## UTANGULIZI

Uchaguzi wa haki, huru, amani na wa kuaminika hutegemea ushirikiano na uadilifu wa wadau muhimu wa uchaguzi katika kutekeleza wajibu wao wakati wa kuendesha kampeni na zoezi la uchaguzi. Kwa kuzingatia kifungu cha 162 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyama vyote vya siasa imeandaa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi kwa lengo la kuweka msingi unaopaswa kuzingatiwa na washiriki wa uchaguzi pamoja na hatua za kinidhamu zinazoweza kuchukuliwa kwa atakayekiuka Kanuni hizi.

Jitihada za wazi na za makusudi zifanyike kuhakikisha kuwa Kanuni hizi zinazingatiwa na kuheshimiwa na wahusika wote. Hivyo, wahusika wa maadili haya watahakikisha kuwa Kanuni hizi zinafahamika na kuzingatiwa na wanachama wa vyama vya siasa, wafuasi na wadau wote wa uchaguzi.

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 Jina, Lengo, Matumizi, Wahusika na Wajibu wa Kusaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za Mwaka 2025

### 1.1 Jina la Kanuni

Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025.

### 1.2 Lengo la Maadili

Kanuni za Maadili zinaweka msingi unaopaswa kuzingatiwa na washiriki wa uchaguzi pamoja na hatua za kinidhamu zinazoweza kuchukuliwa kwa atakayekiuka Kanuni hizi.

### 1.3 Muda wa Kutumika kwa Kanuni za Maadili

Kanuni hizi za Maadili zitatumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, kuanzia siku moja baada ya tarehe ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi mkuu hadi baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi huo. Vilevile, Kanuni hizi zitatumika katika chaguzi ndogo zitakazofuata.

### 1.4 Wahusika wa Kanuni za Maadili

Wahusika wa Kanuni hizi za Maadili ni wafuatao: -

(a) vyama vya siasa;

(b) wagombea;

(c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(d) Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

**1.5 Wajibu wa Kusaini na Kuthibitisha Kuheshimu Kanuni za Maadili**

(a) Kila chama cha siasa, Serikali na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi watawajibika kusaini Kanuni hizi za Maadili. Chama cha siasa ambacho hakitasaini Kanuni hizi za Maadili kitazuiliwa kushiriki katika uchaguzi.

(b) Kila mgombea, kabla ya kuteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi atathibitisha kuheshimu na kutekeleza Kanuni hizi za Maadili kwa kujaza na kusaini Fomu Na.10 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 mbele ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi kadiri itakavyokuwa. Fomu hiyo itatolewa na Tume au msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi na itarejeshwa pamoja na fomu ya uteuzi.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 Maadili kwa Vyama vya Siasa na Wagombea Katika Kuendesha Shughuli za Siasa Wakati wa Kampeni hadi Kutangazwa kwa Matokeo

#### 2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea

Vyama vya siasa na wagombea watakuwa na wajibu ufuataao: -

(a) kuheshimu na kufuata Katiba ya nchi, sheria za uchaguzi, kanuni za uchaguzi, Kanuni za Maadili ya Uchaguzi na maelekezo ya Tume pamoja na sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha uchaguzi;

(b) kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwasisitiza wanachama wao kuheshimu na kufuata sheria za uchaguzi, sheria nyingine za nchi, kanuni na taratibu zilizowekwa;

(c) kuhakikisha kuwa, mikutano ya kampeni inazingatia ratiba rasmi iliyoratibiwa na Tume, wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi katika kutangaza sera zao;

(d) kuhakikisha kuwa wanazingatia muda wa kuanza na kumalizika kwa kampeni ambapo mikutano yote itafanyika kati ya saa 2:00 asubuhi na saa 12:00 jioni. Bila kuathiri muda ulioelezwa hapo juu, vyama vya siasa vinaweza kutumia vipaza sauti kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 2:00 usiku kwa ajili ya kutoa matangazo ya mikutano itakayofuata;

(e) kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kuwa hakuna migongano ya ratiba za mikutano ya kampeni katika eneo moja. Iwapo ratiba za mikutano zitagongana, wawakilishi wao watakutana na Tume au msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi kutatua changamoto hiyo kwa amani bila kutumia nguvu, vitisho au vurugu;

(f) kuhakikisha kuwa, misafara ya kampeni ya chama kimoja cha siasa haikutani na misafara ya kampeni ya chama kingine cha siasa;

(g) kuhakikisha vyama vyote vya siasa, viongozi wa vyama vya siasa, wagombea, wanachama na wafuasi wao wanachukua hatua za makusudi kwa mujibu wa sheria kuhakikisha kwamba: -

(i) uchaguzi unakuwa wa haki, huru na amani;

(ii) vitendo vinavyoashiria vurugu na vitisho vinaepukwa;

(iii) aina yoyote ya ubaguzi kwa misingi ya jinsia, ulemavu, ukabila, mahali mtu anapotoka, udini, maumbile au rangi unakataliwa na kuepukwa;

(iv) taarifa kuhusiana na uchaguzi na mchakato wa uchaguzi zinazotolewa ni sahihi; na

(v) wanazingatia sheria na kanuni zinazosimamia matumizi ya vyombo vya habari na mitandao

ya kijamii katika kutekeleza shughuli za uchaguzi.

(h) kuhakikisha kuwa, vijitabu, vipeperushi, vitini, mabango na machapisho ya aina yoyote yatakayotumika kuelezea sera zao yatatumika tu na vyama vya siasa, wagombea, wanachama na wafuasi wao baada ya kuidhinishwa na Tume kwa upande wa uchaguzi wa Rais na msimamizi wa uchaguzi kwa upande wa uchaguzi wa wabunge na madiwani;

(i) kutumia vyombo vya habari vya umma kutangaza sera zao kwa kuzingatia Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, na maelekezo ya Tume. Vyombo hivyo vinaweza kutumiwa na wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na makamu wa Rais na kugharamiwa na Serikali;

(j) kuhakikisha kuwa wanajenga mazingira yatakayowezesha uchaguzi kufanyika kwa uhuru na haki, ikiwa ni pamoja na kuwezesha makundi mbalimbali ambayo katika Kanuni hizi, yanajumuisha wazee, wajawazito, wapiga kura wenye watoto wachanga, wanawake na watu wenye ulemavu kushiriki vyema katika uchaguzi;

(k) kushirikiana na watendaji wa uchaguzi kuhakikisha upigaji kura unakuwa wa amani na utulivu ili wapiga

kura wawe huru kutumia haki yao ya kupiga kura bila usumbufu, bughudha au vitisho;

(l) kuhakikisha kuwa, chama cha siasa, mgombea au wafuasi wa chama cha siasa wanapotaka kufanya maandamano wakati wa uchaguzi wanafuata masharti ya sheria husika;

(m) kushirikiana na wafuasi wao kutunza usafi wa mazingira wakati wa kusambaza matangazo ya kampeni. Aidha, kila chama cha siasa kitawajibika kuondoa mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote yaliyotumika wakati wa kampeni katika maeneo ya wazi mara tu baada ya uchaguzi;

(n) kuhakikisha kuwa, lugha ya Kiswahili itakuwa ndio lugha itakayotumika katika kampeni za uchaguzi. Iwapo lugha hiyo haieleweki, na itakapolazimu, mgombea atazungumza katika lugha ya Kiswahili na mkalimani atatafsiri katika lugha inayoeleweka kwa jamii husika;

(o) kutoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika pindi wanapofahamu tukio lolote linaloweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani;

(p) kuhakikisha kuwa, kampeni zinazofanyika ama na wao wenyewe au kupitia wafuasi na wanachama wao zinazingatia misingi inayolenga kutangaza sera zao na kwamba hazijengi chuki na mifarakano miongoni mwa wananchi, viongozi na Serikali;

(q) kuwakataza wanachama au wafuasi wao kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara ya vyama vyao vya siasa au kuvaa sare zenye rangi ya chama chao cha siasa katika mikutano ya hadhara ya vyama vingine vya siasa;

(r) kuhakikisha kuwa, wanafuata utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko uliowekwa kwa mujibu wa sheria iwapo hawakuridhika na mwenendo wa uchaguzi. Katika kipindi cha kampeni malalamiko yawasilishwe kwenye kamati husika ya maadili ya uchaguzi; na

(s) kuwaelimisha na kuwaelekeza mawakala wao watakaokuwepo katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za uchaguzi, kanuni za uchaguzi, taratibu na maelekezo ya Tume.

**2.2 Mambo Yasiyotakiwa Kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea**

Vyama vya siasa na wagombea hawatapaswa kufanya mambo yafuatayo: -

(a) kufanya fujo au kuchochea vurugu ya aina yoyote katika mikutano ya vyama vingine vya siasa;

(b) kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, ulemavu, rangi au maumbile kwenye mikutano na kwenye shughuli zote za kampeni;

(c) kufanya kitendo chochote cha unyanyasaji au ukatili wa kijinsia kwa mgombea kinyume na masharti ya kifungu cha 135 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024. Vitendo vya unyanyasaji na kijinsia kwa mujibu wa kipengele hiki vitajumuisha-

   (i) matumizi ya picha zinazoweza kudhalilisha au kutweza utu wa mtu;
   (ii) kugusa sehemu za maumbile ya mwili wa mtu kwa lengo la kudhalilisha utu wake;
   (iii) kutumia maneno yanayolenga kudhalilisha mtu wa jinsi fulani; au
   (iv) kufanya kitendo chochote ambacho kinaweza kutafsiriwa kuwa ni ukatili au unyanyasaji wa kijinsia.

(d) kuruhusu viongozi, wagombea, wanachama na wafuasi wao kubeba silaha yoyote ikiwa ni pamoja na silaha za jadi au zana yoyote inayoweza kumdhuru mtu katika mikutano na shughuli zote za kampeni au mkusanyiko wowote wa kisiasa;

(e) kufanya au kuruhusu wafuasi na wanachama wao kufanya kampeni kwenye majengo ya ibada na kuwatumia viongozi wa dini kufanya kampeni;

(f) kuwa na, au kubeba sanamu, kinyago, picha au kitu chochote ambacho kinaonesha kudhalilisha, kukebehi au kufedhehesha chama kingine cha siasa au kiongozi wake au Serikali katika mkutano au mkusanyiko wowote wa kisiasa;

(g) kutumia vipaza sauti au kuruhusu viongozi, wanachama au wafuasi wao kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa

shughuli za kisiasa nyakati zote za usiku kuanzia saa 2:00 usiku hadi saa 12:00 asubuhi;

(h) kubandua, kuharibu au kuchafua matangazo ya kampeni ya vyama vingine vya siasa na matangazo ya uchaguzi yanayotolewa na Tume au kutumia viongozi, wanachama au wafuasi wao kufanya hivyo;

(i) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au michoro yoyote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;

(j) kukosoana kwa tuhuma zisizokuwa na uthibitisho bali ukosoaji ujikite katika sera, programu na kazi zao walizofanya;

(k) kuomba kupigiwa kura kwa misingi ya udini, ukabila, au mahali mtu anapotoka, jinsi au rangi;

(l) kutokubali au kutokuheshimu uamuzi wa Tume unaofanywa kwa mujibu wa sheria za uchaguzi;

(m) kutoa rushwa au fadhila ili kumshawishi mtu kusimama kama mgombea au kujitoa ugombea wake au kutumia viongozi, wanachama au wafuasi kufanya hivyo;

(n) kuzuia watu kuhudhuria mikutano ya kampeni ya vyama vingine vya siasa au kutumia wanachama au wafuasi wao kufanya hivyo;

(o) katika siku ya upigaji kura, vyama vya siasa, wagombea, wanachama au wafuasi wao kukodi au kutumia usafiri wa

aina yoyote kubeba wapiga kura kwa madhumuni ya kuwashawishi kumpigia kura mgombea fulani;

(p) kutumia mitandao ya kijamii kufanya kampeni za chuki, uchochezi, udhalilishaji au ubaguzi wa kijinsia; na

(q) kuingilia majukumu ya kamati za maadili.

**2.3 Maadili Wakati wa Upigaji Kura Hadi Kutangaza Matokeo ya Uchaguzi**

**2.3.1 Mambo yanayotakiwa kufanywa na vyama vya siasa na wagombea**

Vyama vya siasa na wagombea wakati wa upigaji kura hadi kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi pamoja na mambo mengine watahakikisha kuwa: -

(a) mawakala wao wanaapa kiapo cha kutunza siri siku saba kabla ya upigaji kura au ndani ya kipindi kifupi kama Tume itakavyoruhusu;

(b) kunakuwa na ushirikiano baina ya vyama vya siasa, mawakala wa vyama vya siasa, wagombea na watendaji wa uchaguzi katika vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume. Hii, itawezesha zoezi la upigaji kura kufanyika kwa amani na utulivu;

(c) viongozi wa vyama vya siasa wanawaelimisha na kuwasisitiza wanachama wao kuwa, mara wanapomaliza kupiga kura waondoke vituoni ili

kuepusha msongamano na vitendo vinavyoweza kuchochea uvunjifu wa amani;

(d) wanawaelimisha mawakala wa vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi kuwa wanaruhusiwa kusindikiza masanduku ya kura hadi kufikishwa mahali pa kujumlishia kura kwa kuzingatia maelekezo ya Tume; na

(e) wanafuata na kutekeleza maamuzi na maelekezo ya Tume pamoja na kukubali na kuheshimu matokeo ya uchaguzi. Aidha, malalamiko yoyote yatakayojitokeza yafikishwe kwenye mamlaka inayohusika kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

**2.3.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na vyama vya siasa**

Mambo yasiyotakiwa kufanyika wakati wa upigaji kura hadi kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi ni pamoja na-

(a) vyama vya siasa, wagombea, wanachama na wafuasi wao katika siku ya kupiga kura kufanya kampeni ya aina yoyote ikiwa ni pamoja na kuvaa vazi lolote au kuonesha ishara yoyote au kuwa na kitu chochote kinachoashiria kushawishi watu kumpigia kura mgombea fulani. Hii, ni pamoja na matumizi ya vyombo vya usafiri vilivyokuwa vinatumika wakati wa kampeni vinavyoashiria utambuzi wa chama fulani cha siasa;

(b) viongozi wa vyama vya siasa, wagombea, wanachama au wafuasi wao kufanya vitendo vinavyoweza kusababisha fujo na vurugu katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(c) mtu yeyote kutumia simu ya kiganjani au kifaa kingine cha mawasiliano ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia au kujumlishia kura isipokuwa msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi, msimamizi wa kituo, wasaidizi wake na mlinzi wa kituo cha kupigia kura ambao watatumia simu zao au kifaa kingine cha mawasiliano pale itakapobidi kwa shughuli za uchaguzi tu na simu au vifaa hivyo wakati wote viwe vimeondolewa mlio na viwe kwenye mtetemo (*vibration*);

(d) kiongozi, mgombea au mtendaji wa chama cha siasa, mwanachama au mfuasi kujihusisha na vitendo vifuatavyo: -

  (i) kuwahamasisha wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja katika uchaguzi mmoja;

  (ii) kununua kadi ya mpiga kura, kukusanya kadi za wapiga kura au kuharibu kura;

  (iii) kutoa hongo, zawadi, kununua kura, shukrani au aina yoyote ya malipo ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au mtendaji wa uchaguzi; na

(iv) kuhamasisha au kuzuia wapiga kura wasijitokeze kupiga kura siku ya kupiga kura.

(e) kiongozi, mgombea au mtendaji yeyote wa chama cha siasa kutoa lugha ya matusi kwa mtendaji wa uchaguzi; na

(f) kiongozi au mtendaji wa chama cha siasa, mwanachama au mfuasi kuvamia au kukaa kwa nguvu ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia au kujumlishia kura.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 Maadili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### 3.1 Wajibu wa Serikali

Wakati wa uchaguzi, Serikali itakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa uchaguzi, hususan, vyama vya siasa ili kuendesha shughuli zao za kisiasa kwa uhuru na kwa kuzingatia sheria za nchi;

(b) kuendelea kuwahudumia wananchi kwa usawa bila kujali uanachama au imani yao kwa vyama vya siasa;

(c) kuhakikisha kuwa kuna hali ya usalama, amani na utulivu katika kipindi chote cha uchaguzi. Aidha, vyombo vya usalama vitoe ulinzi wakati wa mikutano ya kampeni na wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha usalama, amani na utulivu unakuwepo. Vyombo hivyo vizingatie mahitaji na usalama wa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu, wanawake, wazee, wajawazito na wapiga kura wenye watoto wachanga;

(d) kutoa fursa sawa kwa vyama vya siasa vyenye wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais kutumia vyombo vya habari na utangazaji vinavyomilikiwa na Serikali ili kutangaza sera zao; na

(e) kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa mamlaka na madaraka yao katika shughuli za uchaguzi.

### 3.2 Yasiyotakiwa Kufanywa na Serikali

Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Serikali wakati wa uchaguzi ni pamoja na-

(a) kuingilia au kuzuia isivyo halali mikutano iliyoitishwa na vyama vya siasa au wagombea kwa mujibu wa ratiba za uchaguzi;

(b) vyombo vya ulinzi na usalama kutumia mamlaka yake kukandamiza wagombea, wafuasi au chama chochote cha siasa. Aidha, vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake kwa kuzingatia sheria, haki na weledi; na

(c) kumhamisha mtumishi yeyote wa Serikali anayehusika na shughuli za uchaguzi mpaka mchakato wa uchaguzi ukamilike. Endapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaona kuna ulazima wa kumhamisha mtumishi kama huyo ni inapaswa kushauriana na Tume.

### 3.3 Mambo Yasiyotakiwa Kufanywa na Watendaji wa Serikali Wakati wa Uchaguzi

Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Serikali wakati wa uchaguzi ni pamoja na;

(a) Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuchanganya ziara za kikazi na shughuli za kiuchaguzi na kutumia vyombo au watendaji wa Serikali katika shughuli za uchaguzi kwa manufaa yao;

(b) kuanzia kipindi cha kampeni za uchaguzi hadi kutangazwa kwa matokeo Mawaziri hawaruhusiwi-

(i) kutangaza katika vyombo vya habari au kwa namna yoyote misaada au ahadi ya aina yoyote;

(ii) kutoa ahadi za shughuli za maendeleo ya jamii kwa mfano, kujenga barabara, kusambaza maji na mambo mengine kama hayo kwa lengo la kuungwa mkono kisiasa; na

(iii) kutumia madaraka au rasilimali za Serikali kwa shughuli za kampeni za uchaguzi kwa manufaa ya chama chochote cha siasa au mgombea yeyote;

(c) Waziri au afisa mwandamizi yeyote wa Serikali kumwita msimamizi wa uchaguzi kwa lengo la kujadili au kutoa maelekezo kuhusu masuala ya uchaguzi kuanzia kipindi cha kampeni hadi kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi; na

(d) Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine wa Serikali kuingia katika vituo vya kupigia, kuhesabia au kujumlishia kura. Isipokuwa kwamba Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine wa Serikali wanaruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura kwa madhumuni ya kupiga kura tu.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 Maadili kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

### 4.1 Yanayotakiwa Kufanywa na Tume

Mambo yanayotakiwa kufanywa na Tume ni pamoja na: -

(a) kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sheria za uchaguzi na sheria nyingine za nchi;

(b) kupanga, kusimamia na kuendesha uchaguzi katika misingi inayowezesha uchaguzi kuwa huru na wa haki;

(c) kuvipatia vyama vya siasa ratiba na taarifa za uchaguzi kwa wakati;

(d) kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kusimamia na kuratibu taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu ya mpiga kura. Aidha, utoaji wa elimu ya mpiga kura utazingatia mahitaji maalum;

(e) kutoa mafunzo ya kutosha kwa watendaji wanaohusika na uchaguzi ili kuwawezesha kusimamia na kuratibu uchaguzi kwa ufanisi. Mafunzo hayo yatajumuisha elimu ya jinsia na namna ya kuwahudumia wanawake, wazee na watu wenye ulemavu;

(f) kuvipatia kwa wakati vyama vya siasa kanuni, maelekezo ya Tume, nakala ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na nyaraka nyingine za uchaguzi zinazotakiwa;

(g) kukemea vitendo vyenye nia ya kuharibu uchaguzi vinavyoweza kufanywa na viongozi wa vyama vya siasa,

wagombea, wanachama na wafuasi wao, Serikali, watendaji au vyombo vyake;

(h) kuratibu matumizi ya vyombo vya habari vya umma ili kutoa fursa sawa kwa wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais na Makamu wa Rais na vyama vyao vya siasa;

(i) kuendesha zoezi la uchaguzi kwa uwazi na uadilifu;

(j) kuratibu uendeshaji wa kamati za ratiba za kampeni za wagombea;

(k) kuratibu kamati za kusimamia maadili ya uchaguzi pamoja na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na kamati hizo;

(l) kukutana na wawakilishi wa vyama vya siasa mara kwa mara pale itakapowezekana kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na kampeni za uchaguzi na uchaguzi wenyewe;

(m) kuhakikisha kuwa hakuna mtendaji wa uchaguzi atakayefanyiwa uonevu au kukoseshwa haki kutokana na utendaji wake katika shughuli za uchaguzi anazozifanya kwa mujibu wa sheria;

(n) kuhakikisha kwamba watendaji wa uchaguzi wanatambua majukumu ya mawakala na wagombea na haki yao ya kuwasilisha pingamizi au malalamiko iwapo ukiukwaji wa sheria na taratibu umetokea;

(o) kuhakikisha kwamba katika kipindi cha uteuzi wa wagombea, upigaji kura na katika hatua yoyote ya mchakato

wa uchaguzi, watendaji wa Tume wanakuwepo katika maeneo yao ya kazi wakati wote;

(p) kuhakikisha kwamba watendaji wa uchaguzi wanatekeleza jukumu la kutoa na kupokea fomu za rufaa kwa niaba ya Tume; na

(q) kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa vya kutosha kwenye vituo vya kupigia kura na kuhakikisha vifaa hivyo vinatunzwa katika hali ya usalama.

## 4.2 Yasiyotakiwa Kufanywa na Tume

Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Tume ni pamoja na-

(a) kupendelea chama chochote cha siasa au mgombea yeyote;

(b) kubadili ratiba za kampeni za uchaguzi bila kushirikisha vyama vya siasa;

(c) kuchelewa au kupeleka vifaa pungufu katika vituo vya kupigia kura bila sababu za msingi;

(d) kuchelewa kufungua vituo bila sababu ya msingi; na

(e) kuchelewa kutangaza matokeo ya uchaguzi bila sababu za msingi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 Usimamizi na Utekelezaji wa Maadili ya Uchaguzi

### 5.1 Kamati za Maadili

Kamati za maadili zitakazosimamia utekelezaji wa maadili ya uchaguzi zitakuwa kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ya Rufaa;
(b) Kamati ya Kitaifa;
(c) Kamati ya Jimbo; na
(d) Kamati ya Kata.

### 5.2 Muundo na Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi

### 5.2.1 Kamati ya Rufaa

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa kutoka Kamati ya Kitaifa na itaundwa na-

(a) Mwenyekiti ambaye ni Mwenyekiti wa Tume;
(b) Makamu Mwenyekiti ambaye ni Mjumbe wa Tume;
(c) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais ambaye ni Mwenyekiti au Katibu Mkuu au mwakilishi wa chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais;
(d) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu au mwakilishi wake; na
(e) katibu wa Kamati ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi au mwakilishi wake na katibu msaidizi wa kamati ambaye ni miongoni mwa maafisa waandamizi wa sekretarieti ya Tume.

Wakati wa kikao cha kamati, katibu au katibu msaidizi atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

**5.2.2 Kamati ya Kitaifa**

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa Rais na rufaa kutoka kamati ya jimbo. Kamati hii itaundwa na-

(a) Mjumbe mmoja wa Tume ambaye atakuwa Mwenyekiti wa kamati;

(b) mwakilishi mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais. Aidha, mwakilishi huyo atapaswa kuwasilisha kwa mwenyekiti wa kamati barua ya uteuzi kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama husika cha siasa;

(c) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu; na

(d) Katibu na katibu msaidizi wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi kutoka miongoni mwa maafisa waandamizi wa sekretarieti ya Tume.

Wakati wa kikao cha kamati, katibu au katibu msaidizi atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

**5.2.3 Kamati ya Jimbo**

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa ubunge katika jimbo husika pamoja na kusikiliza rufaa kutoka kamati ya maadili ngazi ya kata. Kamati hii itaundwa na: -

(a) msimamizi wa uchaguzi katika jimbo ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati;

(b) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi katika jimbo husika ambaye atawasilisha barua ya utambulisho kwa mwenyekiti wa kamati kutoka kwa katibu wa wilaya au mkoa wa chama husika cha siasa;

(c) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na katibu tawala wa wilaya husika; na

(d) katibu wa kamati ambaye atakuwa ni msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo.

Wakati wa kikao cha Kamati ya Maadili, katibu wa kamati atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

### 5.2.4 Kamati ya Kata

Kamati hii itasikiliza malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa udiwani katika kata husika na itaundwa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi baada ya kupata maelekezo kutoka Tume. Kamati hii itaundwa na: -

(a) Mwenyekiti wa kamati ambaye ni msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata;

(b) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki katika uchaguzi kwenye kata husika ambaye atawasilisha barua ya utambulisho kwa mwenyekiti wa kamati kutoka kwa katibu wa wilaya au kata wa chama husika cha siasa;

(c) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na katibu tawala wa wilaya husika; na

(d) Katibu wa kamati ya maadili ya uchaguzi atatoka katika ofisi ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya Kata.

Wakati wa kikao cha kamati ya maadili ya uchaguzi, katibu wa kamati atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

**5.3 Kamati za Maadili kwa Mgombea Pekee wa Urais, Ubunge au Udiwani**

Endapo kuna mgombea pekee wa Urais, Ubunge au Udiwani, kamati za maadili zilizoanishwa katika aya ya 5.1 zitatumika na utaratibu ulioanishwa katika sehemu hii utatumika. Isipokuwa kwamba kamati hizo zitaundwa na mjumbe mmoja kutoka kwenye chama cha siasa chenye mgombea pekee, Serikali na Tume.

**5.4 Kamati za Maadili Wakati wa Uchaguzi Mdogo**

Kutakuwa na kamati za maadili wakati wa uchaguzi mdogo kama ifuatavyo: -

5.4.1 Endapo uchaguzi mdogo unafanyika katika kata, kamati itabaki kama ilivyo katika aya ya 5.2.4 na itaundwa kamati ngazi ya jimbo kwa ajili ya kupokea rufaa kutoka ngazi ya kata.

5.4.2 Endapo kutakuwa na uchaguzi mdogo wa ubunge, kamati itakayotumika ni kama ilivyo katika aya ya 5.2.3 na itaundwa kamati ya kitaifa kwa ajili ya kupokea rufaa kutoka ngazi ya jimbo.

**5.5 Uwasilishaji wa Malalamiko**

Mgombea yeyote, Tume, Serikali au chama cha siasa kilichosaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi na kuweka mgombea iwapo kinaamini kwamba maadili ya uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko yake kwa mwenyekiti wa kamati ya maadili ya uchaguzi katika ngazi husika kwa maandishi. Aidha, malalamiko kuhusu ukiukwaji wa maadili kwa mgombea pekee yatawasilishwa na Tume.

Isipokuwa kwamba changamoto au malalamiko yoyote kuhusiana na mchakato au taratibu za uchaguzi yatakayojitokeza siku ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura, yatawasilishwa kwa maandishi kwa msimamizi wa kituo kupitia kwa wakala.

**5.6 Muda wa Kuwasilisha Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili**

Malalamiko yoyote yatakayotokea yatawasilishwa kwa maandishi kwa mwenyekiti wa kamati ya maadili ya uchaguzi ya ngazi husika ndani ya saa sabini na mbili (72) tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**5.7 Kuitisha Kikao cha Maadili ya Uchaguzi**

Mwenyekiti wa kamati husika baada ya kupokea malalamiko anatakiwa kuitisha kikao ndani ya saa arobaini na nane (48).

**5.8 Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko**

Malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa maadili yatashughulikiwa kwa utaratibu ufuatao: -

(a) malalamiko yote yatajadiliwa na kuamuliwa katika kikao cha kamati ya maadili ya uchaguzi kwenye ngazi husika;

(b) kamati itashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi wake mapema iwezekanavyo;

(c) baada ya kupokea malalamiko, Kamati itamtaka anayelalamikiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya saa arobaini na nane (48) tangu kupokea taarifa ya malalamiko dhidi yake;

(d) kamati, katika kushughulikia malalamiko, inaweza kumuita mtu yeyote kutoa maelezo au ushahidi ili kuisaidia kamati kufikia uamuzi wa haki;

(e) akidi ya kikao cha kamati husika itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa kamati;

(f) kamati itaamua malalamiko yote ndani ya muda wa saa arobaini na nane (48) baada ya kusikiliza au kupata maelezo ya utetezi kutoka kwa pande zote mbili ambazo ni mlalamikaji na mlalamikiwa;

(g) uamuzi utakaofikiwa na kamati ya maadili ya uchaguzi utatekelezwa na pande zinazohusika na maamuzi hayo;

(h) ikitokea kuna umuhimu wa kufanya uamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa mlalamikaji na mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura juu ya uamuzi huo;

(i) malalamiko yatakayoshughulikiwa na kamati ya maadili ya uchaguzi ni yale ya kipindi cha kampeni za uchaguzi tu;

(j) malalamiko yatakayotokea siku ya upigaji kura yatashughulikiwa na msimamizi wa kituo cha kupigia kura,

msimamizi msaidizi wa uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi au Tume kwa mujibu wa sheria za uchaguzi;

(k) kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yatakayowasilishwa kabla ya kufanya uamuzi; na

(l) kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kupelekwa kwenye mamlaka husika kama itakavyoona inafaa.

**5.9 Rufaa Dhidi ya Uamuzi wa Kamati**

Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa kamati ya maadili ya uchaguzi una haki ya kukata rufaa kwa taratibu zifuatazo: -

(a) kama ni malalamiko yaliyoshughulikiwa katika ngazi ya kata, rufaa itakatwa kwenda kwa msimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya maadili ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu uamuzi unaokatiwa rufaa ulipotolewa;

(b) uamuzi utakaotolewa na kamati ya jimbo utakuwa ni wa mwisho kwa malalamiko yote yaliyoanzia ngazi ya kata;

(c) iwapo malalamiko yaliyoshughulikiwa ni kutoka ngazi ya jimbo, rufaa itakatwa kwenda kwa mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kitaifa ndani ya saa arobaini na nane (48) tangu uamuzi husika ulipotolewa;

(d) uamuzi wa Kamati ya Kitaifa utakuwa ni wa mwisho kwa malalamiko yote yaliyoanzia ngazi ya jimbo;

(e) iwapo malalamiko yaliyoshughulikiwa ni kutoka Kamati ya Kitaifa, rufaa itakatwa kwenda Kamati ya Rufaa ndani ya saa arobaini na nane (48) baada ya uamuzi wa Kamati ya Kitaifa kutolewa;

(f) iwapo kuna umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa mlalamikaji na mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura ya maamuzi; na

(g) upande usioridhika na maamuzi ya kamati kwenye hatua ya mwisho ya rufaa husika unaweza kufungua malalamiko ya uchaguzi Mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

**5.10 Malalamiko Dhidi ya Tume, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

Utaratibu wa kushughulikia malalamiko dhidi ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi utakuwa kama ifuatavyo:

(a) iwapo malalamiko yaliyowasilishwa ni dhidi ya Tume, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi ambaye ni Mjumbe wa Tume, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi hataendesha kikao hicho, bali wajumbe wa kamati husika watamchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa muda na mwenyekiti wa kamati anapojitoa kuendesha kikao atashiriki kama mlalamikiwa;

(b) malalamiko yote yatakayotolewa dhidi ya Tume au wasimamizi wa uchaguzi na iwapo kamati itaona kuwa Tume au msimamizi wa uchaguzi amekosea itaitaka Tume au msimamizi wa uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo; na

(c) iwapo Tume haitachukua hatua za lazima kurekebisha tatizo hilo, upande usioridhika unaweza kuwasilisha mashauri ya uchaguzi mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

**5.11 Malalamiko Dhidi ya Serikali**

Utaratibu wa malalamiko dhidi ya Serikali utakuwa kama ifuatavyo: -

(a) malalamiko yote yatakayotolewa dhidi ya Serikali na iwapo Kamati itakubaliana na malalamiko hayo itaitaka Serikali kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo; na
(b) iwapo Serikali haitachukua hatua za lazima kurekebisha tatizo hilo, mashauri ya uchaguzi yanaweza kuwasilishwa Mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

**5.12 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi Ngazi ya Kitaifa, Jimbo na Kata Katika Kutoa Adhabu**

Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Kitaifa, Jimbo na Kata zinaweza kuchukua hatua zifuatazo-

(a) kuagiza upande uliokiuka Maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu kuuomba umma msamaha;
(b) kutoa onyo au karipio kwa maandishi;
(c) kutangaza jina la chama cha siasa au mgombea aliyekiuka Maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia ya taarifa

kwa umma kupitia redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano;

(d) kamati inaweza kukisimamisha chama cha siasa au mgombea kuendelea kufanya kampeni za uchaguzi kadiri itakavyoonekana inafaa. Kwa madhumuni ya aya hii, kuzuiwa kufanya kampeni za uchaguzi itajumuisha zuio la kufanya mikusanyiko ya aina yoyote inayoashiria kufanya kampeni za uchaguzi;

(e) kamati inaweza kuzuia chama cha siasa au mgombea kutumia vyombo vya habari au kubandika machapisho ya kampeni kwa muda ambao kamati itaona unafaa;

(f) kukitaka chama cha siasa au mgombea kulipa faini kama ifuatavyo: -

(i) ikiwa ni katika ngazi ya kata, kiasi kisichozidi Shilingi laki mbili (200,000) za Kitanzania ambacho kitathibitishwa na kamati ya jimbo;

(ii) ikiwa ni katika ngazi ya jimbo, kiasi kisichozidi Shilingi laki saba (700,000) za Kitanzania ambacho kitathibitishwa na kamati ya kitaifa; na

(iii) ikiwa ni katika ngazi ya kitaifa, kiasi kisichozidi Shilingi milioni moja na laki tano (1,500,000) za Kitanzania au kwa kadiri kamati itakavyoona inafaa.

(g) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 135 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, adhabu ya kosa la unyanyasaji au ukatili wa kijinsia itakuwa ni kukisimamisha chama cha siasa au mgombea

kufanya kampeni kwa muda ambao kamati itaona unafaa au kulipa faini isiyopungua kiasi cha Shilingi milioni moja (1,000,000) za Kitanzania au vyote.

**5.13 Mamlaka ya Kamati ya Rufaa ya Maadili ya Uchaguzi**

Kamati ya Rufaa ya Maadili ya Uchaguzi inaweza kuchukua hatua zifuatazo katika kushughulikia malalamiko: -

(i) kutoa onyo au karipio;

(ii) kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu kuuomba umma msamaha;

(iii) kutangaza jina la chama cha siasa au mgombea aliyekiuka maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia ya taarifa kwa umma kupitia redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano kama itakavyoonekana inafaa;

(iv) kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kwenye mamlaka husika kama itakavyoona inafaa kwa hatua zinazostahili;

(v) kamati inaweza kusimamisha chama cha siasa au mgombea kuendelea kufanya kampeni za uchaguzi kwa muda kama itakavyoona inafaa;

(vi) kuelekeza chama cha siasa au mgombea kulipa faini isiyozidi Shilingi laki saba (700,000) za Kitanzania kwa ukiukwaji wa Maadili kwa uchaguzi wa ubunge na isiyozidi Shilingi milioni moja na laki tano (1,500,000) za Kitanzania kwa uchaguzi wa urais au kwa kadiri kamati itakavyoona inafaa;

(vii) kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yaliyowasilishwa kwa njia ya rufaa kabla ya kufanya maamuzi;

(viii) faini zote zitakazotozwa katika kamati zote zitalipwa kupitia Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na zitakatiwa risiti; na

(ix) kamati ya Rufaa inaweza kuitisha na kupitia uamuzi uliotolewa na kamati ya kitaifa na inaweza kukubaliana au kubadilisha uamuzi husika.

**5.14 Kushindwa Kutekeleza Maadili**

Endapo mgombea au chama cha siasa kitashindwa kutekeleza maamuzi ya kamati husika, kamati ya rufaa inaweza kukisimamisha chama husika cha siasa kufanya kampeni za uchaguzi.

**5.15 Uamuzi wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Maadili Kutoathiri Haki ya Kufungua Shauri la Uchaguzi**

Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, shauri la uchaguzi halitakataliwa kwa sababu kwamba suala linalolalamikiwa katika shauri hilo lilifanyiwa uamuzi katika mwenendo wa malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa Kanuni hizi:

Isipokuwa kwamba, uamuzi uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi, utakuwa ni ushahidi wa suala linalolalamikiwa katika shauri la uchaguzi.

## SEHEMU YA SITA

### 6.0 Tamko la Kukubali Kanuni za Maadili ya Uchaguzi

Sisi vyama vya siasa, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja tumekubaliana kuwa na uchaguzi huru, wa haki, uwazi, wa kuaminika na wenye kuzingatia ushiriki wa makundi yote katika jamii. Tunaelewa kwamba, amani, ustawi wa nchi, usalama wa raia, uhuru wa vyama vya siasa na utii wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi ndio msingi wa uchaguzi bora. Tunakubaliana kuwajibika kutekeleza Kanuni hizi za Maadili zinazotokana na kifungu cha 162 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024. Hivyo, kwa pamoja tunakubaliana kuweka saini zetu hapa chini kuthibitisha kuwa tutaheshimu na kutekeleza Kanuni za Maadili haya.

### 6.1 Tamko la Serikali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba inakubali na kuahidi kutekeleza Kanuni za Maadili haya ipasavyo.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina: Dr. Jim J. Yonazi
Wadhifa: Katibu Mkuu - OWM, SBU
Saini: [signature]
Tarehe: 12/04/2025

## 6.2 Tamko la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatamka kwamba inakubali na kuahidi kutekeleza Kanuni za Maadili haya ipasavyo.

| | |
|---|---|
| Jina | Jacobs Casthom Mwambegele |
| Wadhifa | Mwenyekiti |
| Saini | |
| Tarehe | 12 Aprili, 2025 |

## 6.3 Tamko la Viongozi wa Vyama Vya Siasa

Mimi kiongozi wa chama cha siasa niliyetia saini hapa chini natamka kwamba ninakubali na kuahidi kutekeleza Kanuni za Maadili haya ipasavyo:-



| NA. | JINA LA KIONGOZI | JINA LA CHAMA CHA SIASA | CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | RASHIDI MOHAMMED RAI | AAFP | K/MKUU | | 12/4/2025 |
| 2. | ADO SHAIBU ADO | ACT - Wazalendo | K/MKUU | | 12/4/2025 |
| 3. | SALEHE M. MSUMARI | ADA-TADEA | K/MKUU | | 12/04/2025 |
| 4. | MWALIMU H. AZIZI | ADC | K/MKUU | | 12/04/2025 |
| 5. | MASOUD ALI ABDALLA | CCK | K/MKUU | | 12/04/2025 |
| 6. | EMMANUEL JOHN NCHIMBI | CCM | K/MKUU | | 12/04/2025 |
| 7. | | CHADEMA | | | |
| 8. | MOHAMMED MASOUD RASHID | CHAUMMA | KATIBU MKUU | | 12/04/2025 |
| 9. | HUSNA MOHAMED ABDALLA | CUF | KATIBU MKUU | | 12/04/2025 |

| NA. | JINA LA KIONGOZI | JINA LA CHAMA CHA SIASA | CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 10. | AMEIR HASSAN AMEIR | MAKINI | K/MKUU | [illegible] | 12-04-2025 |
| 11. | ABDUL JUMA MLUYA | DP | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 12. | EVALINE WILBARD MUNISI | NCCR - Mageuzi | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 13. | DOYO HASSAN DOYO | NLD | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 14. | HASSAN R. ALMAS | NRA | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 15. | MAJALIO P. KYARA | SAU | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025. |
| 16. | YUSTAS M. RWAMUGIRA | TLP | KATIBU MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 17. | SAUM H. RASHID | UDP | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 18. | MOSHI R. KIGUNDULA | UMD | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |
| 19. | HAMAD M. IBRAHIM | UPDP | K/MKUU | [illegible] | 12/04/2025 |

SEHEMU YA SABA

**7.0 Kufuta Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020**

Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 yamefutwa.

Dodoma
12 Aprili, 2025

JACOBS C.M. MWAMBEGELE,
*Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi*